



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA

HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENI



Telegram "REGCOM"

Simu:028-28022872330

Nukushi:028280230

Unapojibu tafadhali taja

Kumb.

Na.HAB.209/250/01C/101

Ofisi ya Mganga Mfawid
S.L.P 16,
KIGOMA.

25 Februari, 2026.

TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni inawatangazia wananchi wote wenye sifa kuomba nafasi za **mkataba wa kujitolea (Volunteer Contract)** katika idara mbalimbali za hospitali kama ifuatavyo:

1. MHUDUMU MOCHWARI (2 Nafasi)

Majukumu:

- i. Kupokea, kuhifadhi na kutoa miili kwa kufuata taratibu za hospitali.
- ii. Kutunza usafi wa chumba cha kuhifadhia maiti na vifaa vyake.
- iii. Kuweka kumbukumbu sahihi za miili inayoingia na kutoka.
- iv. Kushirikiana na wauguzi na madaktari katika utunzaji wa miili.

Sifa za Mwombaji:

- i. Elimu ya kidato cha nne au zaidi.
- ii. Awe na mafunzo au uzoefu wa kazi ya mochwari itakuwa ni faida.
- iii. Awe na nidhamu, uadilifu na uwezo wa kufanya kazi katika mazingira ya changamoto.

2. MTUNZA KUMBUKUMBU (1 Nafasi)

Majukumu:

- i. Kutunza na kupanga mafaili ya wagonjwa na nyaraka za hospitali.
- ii. Kuingiza na kuhifadhi taarifa katika mifumo ya kielektroniki.

All communication must be directed to Medical officer Incharge. Maweni Regional Referral Hospital. P.O.BOX 16. KIGOMA (028-

- iii. Kutoa mafaili kwa wahudumu wa afya kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kuhakikisha usiri wa taarifa za wagonjwa unazingatiwa.

Sifa za Mwombaji:

- i. Diploma ya Utunzaji Kumbukumbu (Records Management) au taaluma inayofanana.
- ii. Ujuzi wa kompyuta (Microsoft Office).
- iii. Uwezo wa kufanya kazi kwa umakini na kwa kufuata maadili ya kazi.

3. DEREVA (2 Nafasi)

Majukumu:

- i. Kuendesha gari la hospitali (ikiwemo gari la wagonjwa – ambulance).
- ii. Kuhakikisha gari linatunzwa na kuwa katika hali nzuri wakati wote.
- iii. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa gari na kuripoti hitilafu.
- iv. Kufata sheria za usalama barabarani.

Sifa za Mwombaji:

- i. Leseni halali ya udereva Daraja C au E.
- ii. Uzoefu wa kuendesha gari kwa angalau miaka 2.
- iii. Cheti cha mafunzo ya huduma ya kwanza (First Aid) kitakuwa ni faida.
- iv. Awe mwaminifu na mwenye nidhamu.

4. MTOA DAWA ZA USINGIZI NA GANZI (ANESTHETIST) (1 Nafasi)

Majukumu:

- i. Kutoa dawa za usingizi na ganzi kwa wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji.
- ii. Kufuatilia hali ya mgonjwa kabla, wakati na baada ya upasuaji.
- iii. Kushirikiana na jopo la upasuaji kuhakikisha usalama wa mgonjwa.
- iv. Kutunza vifaa vya ganzi na kuhakikisha vinafanya kazi ipasavyo.

Sifa za Mwombaji:

- i. Diploma ya utabibu/Uuguzi mwenye cheti cha mafunzo ya Utoaji wa Dawa za Usingizi na Ganzi (Anesthesia).
- ii. Awe amesajiliwa na baraza husika la taaluma ya afya.
- iii. Awe na uzoefu wa kazi hospitalini utakaokuwa ni faida.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Nafasi hizi ni za mkataba wa kujitolea.
- ii. Waombaji wawe tayari kufanya kazi kwa bidii na kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.
- iii. Waambatanishe barua ya maombi, CV, nakala za vyeti na namba ya simu inayopatikana muda wote.
- iv. Maombi yatumwe kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe 6 Machi, 2026 kuanzia saa moja na nusu Asubuhi hadi saa tis ana nusu mchana (1:30 am – 9:30 PM).

Maombi yote yawasilishwe kwa:

Mganga Mfawidhi

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni

S.L.P 16

Kigoma.

Imetolewa na:



Dkt. Joseph E. Nangawe

MGANGA MFAWIDHI
HOSPITALI YA RUFAA YA MAWENI
KIGOMA

MGANGA MFAWIDHI MAWENI RRH